# MUSTAKABALI WA KISWAHILI KATIKA UKANDA WA MAZIWA MAKUU

*Mugyabuso M. Mulokozi*

## 1.0 Usuli

### 1.1 Muktadha

Eneo la Maziwa Makuu hujumuisha nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Somalia (?), Sudan, Tanzania, Uganda, na Zambia.

Kiswahili kilienea katika nchi hizi tangu karne ya 19 kutokana na misukumo ya kiuchumi (biashara na ajira), kisiasa (utawala wa kikoloni, vita) na kitamaduni (shughuli za dini, sanaa, michezo, elimu, n.k.). Kiswahili kilienea kwa sababu kilihitajika.

Hivi leo Kiswahili kinazungumzwa, kwa viwango tofautitofauti, katika nchi hizo zilizotajwa. Jumla ya wazungumzaji wote ni takriban milioni 100. Wengi kati ya watu hao wanazo lugha zao za asili, lakini wapo pia watu kama milioni 10, hususani wakazi wa mijini, ambao hawana lugha nyingine isipokuwa Kiswahili. Idadi ya watu wa aina hiyo, nchini Tanzania, Kenya, Uganda na hata Kongo, inazidi kuongezeka.

Hivi sasa kuna msukumo wa kuleta Umoja zaidi miongoni mwa nchi hizi na hatimaye shirikisho. Kiswahili tayari kimekubaliwa tangu 2004, kutumika rasmi katika vikao vya Umoja wa Afrika (UA). Kuna biashara zaidi, na mwingiliano mkubwa zaidi wa watu. Yote haya yanaashiria mustakabali wenye matumaini kwa lugha ya Kiswahili katika eneo hili.

Makala haya yanatafakari mustakabali wa Kiswahili katika ukanda wa Maziwa Makuu kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo, ambavyo hatimaye ndivyo vitakavyoamua hali ya Kiswahili katika siku zijazo:

- Uchumi
- Utamaduni
- Elimu
- Siasa
- Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)
- Vyombo vya habari
- Utandawazi

Makala yanaangalia pia vikwazo na matishio ya maendeleo na uenezaji wa Kiswahili katika ukanda huu na kupendekeza namna ya kuyakabili.

## 1.2 Mapitio ya Historia

Historia na maendeleo ya lugha ya Kiswahili ilikwishaelezwa vizuri na wataalamu mbalimbali, mathalan Whiteley 1969; Chiraghdin na Mnyampala 1977; Khamisi 1974; 1990; Kiango 2005; Mbaabu 1991; Legere 1990; Massamba 1992; 2002; 2004; Ohly 1982. Hapa hatukusudii kuirudia historia hiyo, bali tutatoa muhtasari tu wa mambo yaliyosaidia kueneza Kiswahili. Mambo hayo tulikwishayaeleza katika makala mengine (rejea Mulokozi 2001), na ni haya yafuatayo:

Kabla ya mwaka 1900 M :

(a) Biashara ya kuvuka bahari;
(b) Biashara na misafara ya kwenda bara, iliyoambatana na ujenzi wa himaya za kiuchumi-kisiasa, k.m. himaya ya Tippu Tip huko Kongo;
(c) Kuenea na kustawi kwa Himaya ya kibiashara ya Sultani wa Zanzibar kuanzia kama mwaka 1832;
(d) Tanzo ya utamaduni wa Kibantu, ambao unajumuisha ule wa Kiswahili; na uvumilivu wake wa mambo mapya ya kigeni ya kitamaduni na kisiasa;
(e) Umoja wa kitamaduni na kilugha wa Waswahili;
(f) Uisilamu.

Miaka ya 1900-1960

Baadhi ya yale yaliyotajwa hapo juu pamoja na haya yafuatayo:

(g) Sera ya lugha ya serikali ya Kidachi (nchini Tanzania Bara, Burundi na Rwanda) ambayo ilikifanya Kiswahili kiwe lugha ya ngazi za chini za utawala, elimu na jeshi;
(h) Shughuli za kimisionari za kueneza Ukristo, ambazo ziliambatana na kuingizwa kwa alfabeti ya kirumi, uchapaji na uchapishaji wa vitabu;
(i) Vita Vikuu vya I na II vya dunia;
(j) Vyombo vya habari, hasa magazeti, magazini, majarida, redio na televisheni (baada ya mwaka 1950);
(k) Shughuli za kitamaduni, hasa utamaduni wa umma, kama vile muziki, michezo, sherehe na miviga, dansi, maigizo na sinema;
(l) Mabadiliko ya kiuchumi, hasa kukua kwa miji, kazi za umanamba, vyama vya wafanyakazi, miundo-mbinu, hasa reli, barabara, na usafiri wa majini;
(m) Siasa za utaifa (vita vya Maji Maji, vita vya Mau Mau, vuguvugu za wafanyakazi na wakulima, kuanzia miaka ya 1920; harakati za kudai Uhuru);
(n) Mfumo wa elimu.

Jambo la msingi ni kwamba maendeleo ya Kiswahili yalitokana na mahitaji, hususani yale ya kiuchumi. Mahitaji ya kiuchumi yana viwango viwili:

kiwango cha uzalishaji, na kiwango cha usambazaji (biashara). Katika kiwango cha uzalishaji, Kiswahili kilikuwa nyenzo ya uzalishaji, hasa katika mashamba makubwa na viwanda. Katika uzalishaji mdogo wa binafsi (wa wakulima, wavuvi na wafugaji vijijini), Kiswahili hakikuwa na dhima kubwa (isipokuwa katika maeneo ya pwani na Visiwani); lugha za makabila zilitumika katika ngazi hizo (isipokuwa wakati wa kuwasiliana na mabwana shamba au kusoma maelekezo kwenye dawa na pembejeo za kilimo. Katika ngazi ya usambazaji na mabadilishano ya bidhaa – ngazi ya biashara – Kiswahili kilitumika zaidi kwa kuwa shughuli hiyo iliambatana na maingiliano na watu wa jamii nyingine wenye kuzungumza lugha tofauti.

Mbali na msukumo wa kiuchumi-kijamii wa kuenea kwa Kiswahili, ambao haukuamuliwa kwa makusudi na mtu yeyote, palikuwa pia na msukumo wa kisiasa-kiutawala wakati na baada ya ukoloni. Serikali za Wadachi nchini *Deutsch Ost-Afrika* (Tanzania Bara ya sasa, Rwanda na Burundi), na Waingereza nchini Tanganyika, Kenya, Zanzibar, na kwa kiasi fulani hata Uganda (ambako Wamisionari na wanajadi walipinga Kiswahili) na Malawi, ziliweka sera ya makusudi ya matumizi ya Kiswahili katika maeneo yaliyoainishwa. Asasi za kusanifisha na kusimamia matumizi ya Kiswahili, kwa mfano *Inter-Territorial Language Committee* (1930) zilianzishwa. Halikadhalika, mashirika ya kuendeleza uandishi na uchapishaji, kwa mfano EALB (1948), yalianzishwa na wakoloni. Huko Kongo msukumo wa kueneza Kiswahili wakati wa ukoloni ulitokana zaidi na juhudi za wamisionari wa Kanisa Katoliki.

Baada ya Uhuru, serikali ziliendelea kutoa msukumo wa matumizi ya Kiswahili. Nchini Kongo, licha ya upinzani mkubwa wa Wafaransa, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha mojawapo ya taifa, kadhalika nchini Uganda mwaka 1973. Nchini Kenya na Tanganyika Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya taifa miaka ya 1960, na kupewa msukumo mkubwa wa kiserikali, hususani katika elimu na utawala, kuanzia miaka ya 1960 nchini Tanzania na miaka ya 1980 nchini Kenya. Siasa ya Ujamaa nchini Tanzania, iliyowaweka pamoja vijijini watu wenye asili mbalimbali; vilevile ilistawisha matumizi ya lugha hiyo nchini. Uganda nayo imeanza kukipa Kiswhaili msukumo wakati wa utawala wa Rais Museveni (kuanzia 1986), na huko Burundi utawala wa sasa unataka kukuza matumizi ya Kiswahili.

Hii ndiyo hali na dhima ya Kiswahili katika eneo la Maziwa Makuu tangu karne ya 19 hadi leo. Hivi sasa dhima ya Kiswahili katika uzalishaji imeanza kufika hata vijijini, hususani nchini Tanzania, na katika maeneo mengine pia imeongezeka sana. Ni muhimu kuzingatia kweli hii tunapotafakari mustakabali wa Kiswahili katika ukanda huu.

## 2.0 Mustakabali wa Kiswahili katika Ukandawa Maziwa Makuu

### 2.1 Uchumi na mustakabali wa Kiswahili

Baadhi ya mambo yaliyosaidia kueneza Kiswahili kabla na wakati wa ukoloni, ambayo tumekwishayaeleza hapo juu, bado yana dhima kubwa katika muktadha wa sasa. Mathalan matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya uchumi katika uzalishaji na katika biashara yanazidi kupanuka. Kuanzishwa kwa viwanda, mashamba makubwa na migodi katika ukanda huu kunawakutanisha watu wa lugha na makabila anuwai, na hivyo kuwalazimisha kutumia Kiswahili ili kuwasiliana.

Katika eneo la Maziwa Makuu, mbali na uchumi wa kawaida wa biashara, kuna uchumi wa uporaji. Huu unadhihirika zaidi katika nchi zenye rasilimali nyingi za madini na mafuta, kwa mfano Kongo, Angola na Sudani. Uporaji huo kwa kawaida unaambatana na vita na machafuko ya kijamii. Vita na machafuko nayo yanakuwa na matokeo ya kueneza Kiswahili, japo hilo si kusudio lake. Mathalan, askari wa Tanzania waliokwenda Uganda kupigana dhidi ya majeshi ya Idi Amin walieneza sana Kiswahili nchini humo. Kadhalika, askari wa Uganda wanaopigana vita Kongo hujikuta wakiishi katika mazingira yenye Kiswahili, na baadhi yao wamerejea Uganda wakiwa na wanawake wa Kikongo wanaozungumza Kiswahili. Upande hasi wa suala hili ni kwamba wakati mwingine Kiswahili kinatumiwa mno na maharamia wanaopora mali na kuua na kujeruhi watu wasio na hatia. Hali hii huwafanya watu wanaoathirika wakichukie Kiswahili kwa kukihusisha na ujambazi, kama ilivyotokea nchini Uganda. Kukua na kupanuka kwa miji, ambako kunakwenda kasi sana, vilevile kunaeneza Kiswahili, maana lugha kuu ya mijini katika ukanda huu ni Kiswahili. Kwa mfano, kwa mujibu wa Shirika la Makazi Duniani la Umoja wa Mataifa (UN-HABITAT), idadi ya wakazi wa mijini nchini Tanzania inakua kwa asilimia 6 kila mwaka (rejea Nipashe 28/1/2006, uk. 7). Watu wanaohamia mijini kutoka vijijini punde huanza kuzungumza Kiswahili, na wale wanaozaliwa mijini hujikuta wakiongea Kiswahili kama lugha yao ya kwanza na ya kila siku. Juhudi za kuleta Shirikisho na umoja wa kikanda, na kuunganisha uchumi wa nchi hizi kwa kuruhusu uwekezaji usiojali mipaka, maingiliano makubwa ya watu, kuondoa ushuru wa forodha, n.k. zinawakutanisha na kuwachanganya watu wa nchi hizi na hivyo kueneza matumizi ya Kiswahili. Iwapo mchakato huu utaendelea, bila shaka Kiswahili kitazidi kustawi.

### 2.2 Utamaduni, Maingiliano ya Kijamii, na Mustakabali wa Kiswahili

Watu wa Afrika Mashariki na Kati ni wamoja; licha ya Kiswahili, lugha zao za asili zinaingiliana sana. Mathalan, Kimasai kinazungumzwa Kenya na Uganda,

Kiluo kinazungumzwa Kenya, Tanzania na Uganda, Kinyarutara kinazungumzwa Tanzania, Uganda na Kongo, n.k.

Mila na desturi za makabila mengi zinafanana, na wakati mwingine sherehe za kimila hufanywa kwa pamoja na wanajamii wa nchi mbili au zaidi (kwa mfano sherehe kuu za kimila za Wamasai). Wananchi wa nchi hizi wanaingiliana na kushirikiana katika mambo mengi, kama vile biashara, kazi, ndoa, elimu, dini, michezo, sanaa (k.m. muziki), fasihi n.k.

Wananchi wanaoishi mpakani huvuka mpaka kila siku kwenda nchi jirani kuuza au kununua bidhaa mbalimbali, na lugha wanayoitumia kwa kawaida ni Kiswahili. Kadhalika, wananchi huvuka mipaka wakitafuta ajira; Tanzania inao wafanyakazi wengi wa aina hiyo kutoka Rwanda, Burundi, Malawi na Kenya. Kadhalika Watanzania wengi wako Kenya, Uganda na kwingineko wanafanya kazi. Maingiliano haya yanapelekea pia katika kuoana, hasa miongoni mwa watu wa mipakani, na hivyo kuungana kifamilia na kilugha, maana wanaooana sharti wazungumze na kuelewana. Watoto na vijana wa Tanzania wanapelekwa kusoma shule nchini Kenya na Uganda. Ingawa lengo la kuwapeleka huko ni pamoja na kujifunza Kiingereza (siyo Kiswahili), lakini athari mojawapo ya misafara hiyo ni kwamba shule nyingi za Uganda, za sekondari na za Juu, mathalan, hivi sasa zimelazimika kufundisha Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao watokao Kenya na Tanzania, na lugha kuu inayotumika nje ya darasa katika baadhi ya shule hizo, na hata katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, ni Kiswahili. Hivyo shule hizi zinaleta mwingiliano kati ya vijana wa Kenya, Uganda na Tanzania, na kujenga mazoea ya kuzungumza Kiswahili. Kwa upande wa dini, viongozi na waumini wa dini za Kiislamu na Kikristo wa nchi hizi wana jadi ya kushirikiana na kufanya ziara za mahubiri, maombi, semina na kadhalika. Ziara za wahubiri wa Kiislamu na wa makanisa ya kilokole za kuzunguka katika nchi hizi zimekuwa ni jambo la kawaida. Aghalabu mahubiri hayo hufanywa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa michezo na sanaa, maingiliano ni makubwa na ya mara kwa mara, na wanamichezo wa nchi hizi wanafahamiana na kushirikiana sana. Wasanii wa muziki wa zamani na wa kizazi kipya hawajui mipaka ya nchi – wanakwenda na kupendwa kotekote ndani ya ukanda huu. Mifano mizuri ni umaarufu wa Watanzania, Lucas Mkenda (Mr Nice), Saida Karoli (Wanchekecha) na Bw. Faustin Munishi nchini Kenya, Uganda na Rwanda; umaarufu wa Mganda, Josse Mayanja (Chameleon), kote Afrika Mashariki, na umaarufu wa mtungaji na mwigizaji wa filamu wa Kenya, Marehemu Ashina Kibibi (wa filamu ya Tausi) nchini Tanzania. Washairi na waandishi wa vitabu vya Kiswahili wa Kenya na Tanzania pia wanafahamiana kiasi, hasa wale walio mashuhuri; kazi za watunzi na wanazuoni mashuhuri wa Kenya, kama Ahmad Nassir, Hassan Mbega, Abdilatif Abdalla, Wallah bin Wallah, Ahmed Sheikh Nabhany, Kimani Njogu, Rocha Chimera, Leo O.

Omolo, n.k. zinasomwa sana nchini Tanzania; na za watunzi wa Tanzania (S. Robert, E.Kezilahabi, Said Ahmed, Adam Shafi, J.K. Nyerere, Amiri Andanenga, M. Mulokozi, n.k.) zinasomwa nchini Kenya. Kwa hakika baadhi ya wasomi wa Kenya wameanza kulalamika kuwa vitabu vya Tanzania vimezidi mno katika shule za Kenya! (King'ei 2000), japo malalamiko hayo yanasahau shabaha muhimu za ushirikiano wetu. Maingiliano haya ya kitamaduni hayatakoma siku za karibuni, na yanaashiria mustakabali mwema wa lugha ya Kiswahili katika ukanda huu.

### 2.3 Elimu na Mustakabali wa Kiswahili

Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya kufundishia elimu ya msingi nchini Tanzania mwaka 1968. Juhudi za kukifanya kiwe lugha ya kufundishia hata elimu ya sekondari na ya juu, zilizoanza tangu mwaka 1969, zimekwamishwa hadi leo, hususani kwa kukosa msukumo wa kiserikali. Nchini Kenya na Kongo Kiswahili kinatumika kufundishia madarasa ya chini katika baadhi ya maeneo, lakini hakifiki darasa la 7 au 8. Hata hivyo, Kiswahili kinafundishwa kama somo katika takriban shule zote za msingi na sekondari nchini Kenya na Tanzania, na katika shule nyingi kiasi nchini Kongo (Mashariki), Burundi, Rwanda na Uganda. Vyuo Vikuu kama 25 vinafundisha Kiswahili katika ukanda huu (10 viko Kenya, 6 Tanzania, 2 Uganda, 1 Burundi, 2 Rwanda, 2 Kongo, 1 Sudan, 1 Msumbiji). Na idadi inazidi kuongezeka. Kenya sasa inatoa wahitimu wa shahada za Kiswahili zaidi ya 2000 kila mwaka katika vyuo vyake vikuu. Tanzania inatoa wachache zaidi – labda hawazidi 500*. Bali kwa jumla tunaweza kusema kuwa wataalamu wa Kiswahili wenye shahada wanaongezeka kila mwaka. Vilevile, walimu wa Kiswahili wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki wanaongezeka, na mwaka 2003 wameunda Chama chao cha Wataalamu wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu (CHAKAMA). Kwa sasa Chama hicho ni cha Afrika Mashariki tu, lakini inatarajiwa kuwa baadaye kitapanua wigo wake hadi Rwanda, Burundi na Kongo. Kiswahili kinafundishwa katika zaidi ya vyuo vikuu 110 duniani. Vyuo 50 kati ya hivyo viko nchini Marekani, vingine kama 30 viko Afrika, 20 viko barani Ulaya, na vilivyosalia vimetawanyika katika nchi mbalimbali za Amerika ya Kusini na Asia. Huko Marekani ziko pia shule nyingi za Weusi zinazofundisha Kiswahili. Hivi karibuni, kutokana na ugomvi wa Al-Qaida na Marekani, juhudi za kufundisha Kiswahili zimeongezwa sana huko Marekani. Kwa ufupi, ni sahihi kudai kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayofundishwa katika vyuo vingi zaidi duniani. Maendeleo haya yanatia matumaini, maana bila ushirikiano miongoni mwa wataalamu wa Kiswahili, na

* Tangu makala haya yaandikwe hali imebadilika. Hivi sasa vyuo viku vya Tanzania vinatoa walimu wa Kiswaili wasiopungua 2000 kila mwaka.

bila kuandaa kizazi kipya cha wazungumzaji wa Kiswahili, hatuwezi kukipatia Kiswahili mustakabali mwema. Hata hivyo, kufundisha tu Kiswahili bila kukitumia kufundishia hakutoshi. Bado kuna haja ya kuongeza juhudi ya kuzishawishi na kuzishinikiza serikali zetu zikubali Kiswahili kiwe lugha ya elimu nchini, angalau nchini Tanzania, Kenya na Ngazija. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuipa lugha ukwasi na mashiko katika ulimwengu wa taaluma, teknolojia, fikira na falsafa, na hivyo kuwa nyenzo ya kuzalisha maarifa zaidi. Mapambano haya inabidi yaendelezwe, hasa siku hizi ambapo hata katika shule za msingi na chekechea nchini Tanzania Kiingereza kimeanza kuchukua nafasi ya Kiswahili!

Rais Benjamin Mkapa alipoingia madarakani mwaka 1995 aliagiza tuendelee kujadili suala la lugha ya kufundishia. Tumelijadili kwa miaka kumi hadi ameondoka! Hatujui awamu mpya itakuwa na msimamo gani juu ya suala hili, japo hatua za kuimarisha Kiswahili zilizoanza kuchukuliwa na serikali ya Mh. Jakaya Kikwete zinatupa matumaini. Jambo la kufurahisha ni kwamba awamu iliyopita imetuachia Sera ya Utamaduni, ambayo inasema:

Mpango maalumu wa kuiwezesha elimu na mafunzo katika ngazi zote kutolewa katika lugha ya Kiswahili utaandaliwa na kutekelezwa (Wizara ya Elimu na Utamaduni, Sera ya Utamaduni, uk. 19).

Mkutano wa kitaifa wa Utamaduni uliofanyika Arusha tarehe 24-28 Mei 1999 uliagiza programu ya utekelezaji wa Sera ya Utamaduni kuhusiana na suala la lugha ya kufundishia iandaliwe mara moja na kuanza kutekelezwa. Je, utekelezaji umekwamishwa na nini? Jibu ni wazi: Umekwamishwa na sera ya lugha ya kufundishia ya Wizara ya Elimu na Utamaduni (kama ilivyokuwa wakati huo). Je, kwa nini Wizara hiyo haitaki Kiswahili kitumike? Jibu wanalo wenyewe, sisi tunaweza kukisia tu. Pengine haya ni baadhi tu ya matokeo ya kuukumbatia kwa pupa utandawazi na uhuria wa biashara na mawazo bila kuwa na msimamo thabiti wa kizalendo kama taifa. [Kuhusu masuala haya, rejea: Mdee, J.S and Mwansoko, H.J.M (wah.) 2000; Kihore, Y & Chuwa, A.R (hakina tarehe); Brock-Utne na wenzake (2004). La muhimu kukumbuka hapa ni kwamba Kiswahili katu hakitastawi na kuchanua katika ukanda huu kama kitabakia kuwa lugha ya sokoni tu bila kuingizwa na kutumiwa katika ngazi za juu za elimu na teknolojia.

## 2.4 Siasa na Mustakabali wa Kiswahili

Katika uwanja wa siasa, michakato miwili ya kisiasa inayotokea katika eneo hili inaweza kusaidia juhudi za kueneza Kiswahili. Mchakato wa kwanza ni ule wa kujenga "demokrasia" ya vyama vingi; na wa pili ni wa juhudi za kuelekea kwenye muungano wa Afrika Mashariki. Mchakato wa vyama vingi na demokrasia, japo ni wa kibwanyenye kisiasa, lakini umesaidia kuwashirikisha watu wengi zaidi, na makundi na mitazamo mingi zaidi, katika siasa. Mijadala

imekuwa mikali zaidi, na lugha kuu ya mijadala hiyo nchini Kenya na Tanzania aghalabu ni Kiswahili. Hata nchini Uganda na Kongo Kiswahili kinatumika sana katika vuguvugu la kisiasa. Ndani ya nchi zenyewe, Kiswahili kinazidi kupata nguvu. Nchini Uganda, Kiswahili kimetangazwa kuwa lugha rasmi pamoja na Kiingereza kuanzia Julai 2005. Uamuzi huu umeongeza hamasa ya kujifunza na kufundisha Kiswahili miongoni mwa Waganda, na hivi sasa wanatafuta walimu na vitabu (niliishuhudia mwenyewe hali hii nilipokuwa Uganda kwenye Tamasha la Vitabu, Oktoba 2005). Ingawa wapinzani wa Kiswahili bado wapo na wana nguvu nchini Uganda, lakini wapenzi pia wanaongezeka, hasa katika muktadha huu wa mchakato wa kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki. Juhudi za kuleta muungano (Shirikisho) wa Afrika Mashariki zimepamba moto miaka ya karibuni, na ratiba ya kuwa na muungano ifikapo kama mwaka 2013 imekwishawekwa. Bunge la Afrika Mashariki tayari lipo, na shughuli za kisiasa ndani ya Afrika Mashariki zinatumia sana Kiswahili. Tayari baadhi ya wabunge wasiofahamu Kiswahili wameanza kujifunza lugha hiyo. Nchi nyingine za ukanda huu, hususani Burundi na Rwanda, pia zimeonyesha nia ya kutaka kujiunga katika Shirikisho. Nchini Kongo "Waswahili" ndio wameshika madaraka, na wanajitahidi kuimarisha matumizi ya lugha hiyo, licha ya matatizo mengi ambayo nchi hiyo inayakabili. Hivyo, licha ya wasiwasi wa Mugambi kuwa Kiswahili nchini Kenya bado hakijawa lugha ya umoja wa kitaifa (Mugambi 1999: 117), dalili zinaonyesha kuwa Kiswahili kitakuwa ndiyo lugha kuu ya umoja wa Afrika Mashariki.

Nje ya ukanda huu, Kiswahili kinazidi kupata nguvu. Kimekubaliwa kuanza kutumika katika Umoja wa Afrika kuanzia Julai 2004. Kinatumika pia katika Bunge la Afrika. Nchi nyingi za Afrika sasa zinaomba walimu. Kiswahili kilikwishateuliwa na Waafrika wa diaspora kuwa lugha yao ya utambulisho tangu miaka ya 1960, na baadhi yao wao wanajaribu kujifunza lugha hiyo na kuwafundisha watoto wao; aidha wanajaribu kupata majina ya Kiswahili kwa ajili yao wenyewe na watoto wao. Sherehe yao ya Kwanzaa imekitwa katika lugha ya Kiswahili.

Waafrika mashuhuri kama Wole Soyinka (tangu miaka ya 1970) na Ayi Kwei Armah (1985) vilevile wamekuwa wakikitetea Kiswahili na kupendekeza kiwe lugha ya bara zima la Afrika. Kulihali siasa za ndani (ya ukanda) zinaonyesha kuwa Kiswahili kinazidi kupendwa, kupewa majukumu zaidi na kupata nguvu. Kikwazo kikubwa cha kisiasa dhidi ya Kiswahili ama kitatoka nje ya ukanda huu, ama ndani ya nchi zenye kuzungumza Kiswahili sana, hususani Tanzania na Kenya. Mathalan, kuna taarifa kuwa hivi majuzi huko Zanzibar imeamuliwa kuwa lugha ya kufundishia shuleni we Kiingereza, badala ya Kiswahili, kuanzia darasa la tano! (rejea Sehemu ya 2.7).

2.5 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mustakabali wa Kiswahili TEHAMA inamilikiwa na kudhibitiwa na mataifa makubwa na makampuni yao, kuanzia hatua za utafiti, hadi uundaji wa vifaa (hadiwea), programu (softiwea) na utumiaji wake. Vyote hivyo vina hataza na hakimiliki lukuki ambazo mtumiaji inabidi azigharimie. Katika hatua ya sasa, TEHAMA ambazo Kiswahili kimejihusisha nazo ni zile za kikompyuta na zile za violezi (audio-visual). Katika eneo la kompyuta, Kiswahili kinaingia kasi. Tayari kuna mamia ya tovuti (webu) za Kiswahili zenye kubeba taarifa muhimu za maarifa, makamusi, matangazo, mafunzo, mfano ni Tovuti ya TUKI <www.udsm.ac.tz/tuki>, na tovuti ya Chuo Kikuu cha Yale: <www.yale.edu/swahili>). Zipo pia injini za upekuzi (search engines) zenye kutumia Kiswahili (mfano: Google). Katika wavuti vile vile Kiswahili kinazidi kupendwa na kutumika. Waafrika Mashariki wengi wanawasiliana kimtandao kwa kutumia Kiswahili.

Zipo na programu maalumu za matumizi (za kimchakato – *processing;* za utumizi – application, za usahihishaji – *spell-checkers* au visahihishi; za uchanganuzi – parsers; za tafsiri za papo kwa papo; na za uchambuzi na uhifadhi wa fasihi/fasihi-simulizi (mfano: Syncrotext ya Smithsonian Institution, Marekani). Baadhi zimetengenezwa Finland, ambao walitangulia kidogo kukiingiza Kiswahili katika programu za kompyuta, baadhi zimetengezwa Marekani, na baadhi zimetengenezwa hapa hapa kwetu. Hivi sasa TUKI inashughulikia miradi sita inayohusiana na kompyuta, ikiwemo miradi ya kufasiri programu-tumizi (Ki-Linux), miradi ya kutengeza kisahihishi na tesauri (spell-checker & thesaurus), miradi ya kutengeneza kamusi na disroma (CD-ROM), za kuhifadhi data za Kiswahili na hata kufundishia Kiswahili, na miradi ya kuhifadhi data za kikompyuta (kanzi), na kutengeneza tafsiri za papo kwa papo.

Mbali na miradi hii ya TUKI, watu na asasi nyingine pia wamo katika kukiingiza Kiswahili katika kompyuta na mifumo ya mawasiliano. Kwa mfano, kampuni ya Microsoft inashirikiana na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufasiri baadhi ya programu zake kwa lugha ya Kiswahili, na makampuni ya simu kama Celtel na Vodacom tayari yanatumia Kiswahili katika mitandao yao. Kadhalika mabenki yenye mashine za fedha yameziprogramu mashine hizo kutumia Kiswahili.

Juhudi hizi ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa Kiswahili kinaendelea kutumika katika ngazi mbalimbali katika ukanda huu. Kama zitaendelezwa na kufanikiwa, bila shaka zitaimarisha matumizi ya Kiswahili kwa siku zijazo.

Kwa upande wa violezi, Kiswahili, kutokana na matumizi yake mapana ya kuweza kuwafikia mamilioni ya watu, kinatumika sana katika teknolojia za

violezi, hasa kanda za muziki, video, redio, filamu za sinema, na vipindi vya televisheni vya burudani na vya kielimu. Matumizi haya yamesaidia kueneza Kiswahili duniani kote. Mathalan waimbaji na waigizaji mashuhuri wa ukanda huu wanatoa kanda na disroma za lugha ya Kiswahili, ambazo zinauzika sana ndani na nje ya ukanda huu.

## 2.6 Vyombo vya Habari, Uchapishaji na Mustakabali wa Kiswahili

Uchapishaji wa magazeti na vitabu kwa lugha ya Kiswahili una historia ndefu ya zaidi ya miaka 100. Hivi sasa magazeti na majarida ya Kiswahili yachapishwayo katika ukanda huu yanazidi 100; mengi yako Tanzania. Uchapishaji wa vitabu nao unasonga mbele, japo si kwa kasi ya kutosha. Jumla ya vitabu vyote vya lugha ya Kiswahili haijulikani, lakini kwa kukisia tu vinaweza kufikia 10,000. Vitabu hivyo ni pamoja na tafsiri kutoka lugha mbalimbali za dunia. Tanzania ndiyo inayochapisha vitabu na magazeti mengi zaidi kwa lugha ya Kiswahili, japo Kenya haiko nyuma sana kwa upande wa vitabu.

Uchapishaji unakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo ya bei kubwa ya karatasi, wino na vifaa vingine, na vikwazo vya mipakani vinavyovuruga biashara ya vitabu kati ya nchi na nchi. Aidha, kuna matatizo ya ufisadi katika manunuzi ya vitabu vya kiada na ziada, waandishi kunyimwa mirabaha yao, soko dogo la wasomaji linaloakisi ukosefu wa utamaduni wa usomaji wa vitabu, n.k. Vyombo vya habari vya kielektroniki, kama vile televisheni, navyo vinaongezeka na vinasaidia kueneza Kiswahili kwa kuwa vinatangaza kwa Kiswahili kwa watu wa ukanda huu. Vituo vya vijana kama kile cha *East African Television* vinapendwa sana kote Afrika Mashariki. Vituo vya redio vimeongezeka sana, vinatumia Kiswahili, na vinasikilizwa na wananchi wengi. Kwa makisio ya haraka nadhani vipo vituo vya televisheni zaidi ya 30 katika ukanda huu vinavyotumia Kiswahili. Magazeti, vitabu, vituo vya redio na televisheni licha ya kutoa habari na maarifa, pia vinawaunganisha watu wa ukanda huu kilugha na kitamaduni, na kueneza matumizi ya lugha ya Kiswahili.

## 2.7 Utandawazi

Istilahi "utandawazi" ilitokana na neno "kutandawaa", yaani kuenea au kusambaa kila mahali. Hivyo utandawazi ni mfumo wa kiulimwengu unaoongozwa na mataifa makubwa tajiri, hususani ya Magharibi, yenye lengo la kuyadhibiti maitaifa yote ya ulimwengu kiuchumi na kitamaduni ili kuyanyonya na kuyatawala kwa faida ya nchi hizo kubwa. Utandawazi kimsingi hauna tofauti na ubeberu. Mbinu za utandawazi takriban ni zilezile za ubeberu wa kawaida, yaani zile za kutumia biashara ya ghiliba, uwekezaji usio na maslahi kwa mwekezwaji, siasa, utamalaki wa kitamaduni, itikadi, ukiritimba wa teknolojia na media ya ulimwengu, vita na uvamizi.

Utandawazi nao una pande mbili; kwa upande mmoja, unaua lugha na tamaduni zetu, bali kwa upande mwingine, unasaidia kustawisha na kutandawaza Kiswahili. Utandawazi unaongeza mawasiliano na maingiliano ya watu na tamaduni. Vyombo vya habari vya kilimwengu vinasambaza habari za Kiswahili duniani kote.

Jukumu letu sisi wakuzaji wa Kiswahili ni kuufanya utandawazi utandawaze Kiswahili.

**3.0 Vikwazo**

Safari ya Kiswahili ya kuwa lugha kuu ya eneo la Maziwa Makuu inakabiliwa na vikwazo vifuatavyo: hali ya uchumi; hadhi ya kisheria ya Kiswahili; ushindani na lugha za kigeni katika utandawazi; utaifa finyu.

Kikwazo kikuu cha ukuaji na ueneaji wa Kiswahili katika ukanda huu ni uchumi dhaifu wa nchi zetu ambao unatulazimisha tuwe tegemezi, na hivyo tukubali kupokea amri kutoka kwa mataifa makubwa, zikiwemo amri za kututaka tukumbatie lugha, imani na tamaduni zao na kuacha zetu. Matabaka tawala ya nchi zetu bado ni dhaifu na hayana msukumo mkubwa wa uzalendo mbali na kutetea matumbo yao. Ni matabaka ya mawakala au vibaraka wa mabepari wa kigeni. Ujenzi wa utaifa imara unahitaji tabaka tawala imara la kizalendo; tabaka hilo linaweza kuwa la kibwanyenye au la kifanyakazi. Kwa wakati huu, matabaka hayo bado yanajijenga.

Kwa sababu ya udhaifu huu, tumekuwa waathirika wa utandawazi badala ya kuwa wafaidika. Kasumba za unyonge na kuiga mambo ya kigeni zimerudi, hatujiamini tena, na tumeanza kuamini kuwa hata lugha na tamaduni zetu hazifai au zimepitwa na wakati. Kwa sababu ya kasumba hii, mara nyingi sisi na viongozi wetu hufanya maamuzi yasiyokuwa sahihi kuhusiana na maslahi yetu halisi na mustakabali wetu.

Lipo vilevile tatizo la kisheria. Kiswahili kinakua kwa nguvu yake chenyewe, na kwa kuwa kinahitajika katika jamii, lakini hakilindwi na nguvu ya kisheria. Kiswahili hakijatajwa katika katiba za nchi zetu (isipokuwa katiba mpya ya Kenya ambayo haijapitishwa), na hakuna sheria au mkataba unaohimiza matumizi na ukuzaji wake katika ukanda huu (japo kinatajwa katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki). Hili nalo inabidi liangaliwe.

Kikwazo cha tatu ni utaifa finyu. Tatizo hili lina ncha tatu. Kwanza kuna ukinzani unaoambatana na ujadi. Kuna watetezi wa lugha za asili ambao hawakubali au hawataki Kiswahili kitumike katika maeneo yao kwa kuwa wanakiona kuwa tishio kwa lugha hizo. Tatizo hili liko zaidi nchini Uganda. Ufumbuzi wa tatizo hili ni kuruhusu lugha za asili zitumike sambamba na Kiswahili bila kuzikandamiza. Hatimaye Kiswahili kitajipenyeza polepole katika lugha hizo hadi kuzisimilisha (au kusimilishwa na lugha hizo). Hili tayari

limeanza kutokea kuhusiana na lugha nyingi za pwani ya Kenya na Tanzania (kwa mfano Kizaramo, Kikwere, Kidigo na Kisegeju).

Pili, kuna mataifa kama Tanzania, Kenya na Ngazija, ambayo yanatamani kukimiliki Kiswahili, na yanaweza kusita au kuogopa kushirikiana na nchi nyingine zinazoongea Kiswahili, ama kwa kuogopa "kuporwa" lugha hiyo, au kwa sababu nyinginezo za utambulisho au maslahi finyu. Ncha ya tatu ni jamii zenyewe za Waswahili wa asili kupenda kukimiliki Kiswahili na kuogopa kuwashirikisha watu wengine wanaotoka nje ya jamii hizo kwa hofu ya ama kushinikizwa ama "kupotoshwa" kwa Kiswahili walichokizoea. Itikadi hii nayo ikiota mizizi huweza kuwa kikwazo cha maendeleo ya Kiswahili, kwani huweza kuwafanya wasio wazawa wa Kiswahili waanze kujihisi kuwa wanajiingiza mahala wasikotakiwa au wanaingilia mambo ya watu. Watu wa aina hiyo wanaweza kukata tamaa na kuamua kurejea katika utaifa finyu wa lugha zao wenyewe za asili. Kinachotakiwa hapa ni sera na msimamo thabiti wa utaifa mpana unaovuka makabila na mataifa ya sasa, na ushirikiano wa wote wenye nia nzuri na mchango wa kutoa katika kukuza Kiswahili.

Tatizo la nne na kubwa sana ni ushindani na lugha za utandawazi, hususani Kiingereza na Kifaransa, na upinzani wa mataifa yenye lugha hizo wa kufanya juhudi zozote za kuibadilisha hali mbaya ya sasa kwa manufaa yetu wenyewe. Utandawazi unawafanya watu wengi waamini kuwa lugha za kigeni ndio ngazi ya kufikia maendeleo, na kwamba maendeleo ni kwenda kufanya kazi Ulaya au Marekani. Adui ana ushawishi na uwezo mkubwa kwa upande wa rasilimali na hata itikadi, na anafanikiwa kuwateka wengi.

**4.0 Hitimisho na Mapendekezo**

Maelezo haya mafupi yamedhihirisha kuwa Kiswahili kinaweza na kinafaa kuwa lugha ya ukanda wa Maziwa Makuu. Mazingira ya kichumi, kijamii na kisiasa yanatupeleka katika hitimisho hilo. Hata hivyo, ili matarajio hayo yatimie, sisi wapenzi na wakuzaji wa Kiswahili hatuna budi kufanya yafuatayo:

(a) Kuendelea kuzishinikiza nchi zetu kukipa Kiswahili nguvu ya kikatiba na kisheria.

(b) Kuhimiza Kiswahili kiwe lugha ya Bunge la Shirikisho la Afrika Mashariki

(c) Kuaandaa wataalamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili kwa kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule na vyuo kote katika eneo la Maziwa Makuu, na kuzishawishi nchi ambazo hazifundishi Kiswahili zifanye hivyo; na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili. Wataalamu hao inabidi tuwasambaze kote ndani na nje ya ukanda huu.

(d) Kushinikiza serikali za Tanzania na baadaye Kenya zikubali Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia elimu ya sekondari, na hatimaye ya juu; na kwa

njia hiyo kukiwezesha kiwe lugha ya sayansi, teknolojia na uanazuoni. Hatua hii itapanua wigo wa lugha ya Kiswahili kutoka sokoni na ngomani hadi katika kumbi za vyuo vikuu na akademia.

(e) Kuweka mkakati wa kukuza uandishi na uchapishaji wa vitabu vya fasihi na vya maarifa kwa kutoa tuzo kwa waandishi, kuwawezesha wachapishaji, kudhibiti uporaji wa hakimiliki, na kutetea haki ya waandishi ya kupata mrabaha na malipo mengine wanayostahiki.

(f) Kuimarisha shughuli za tafsiri na mafunzo ya ukalimani; hususani ni muhimu kufasiri kwa Kiswahili vitabu vingi vya maarifa na fasihi kutoka lugha za kigeni; na kuanzisha mafunzo ya ukalimani katika vyuo vikuu.

(g) Kuimarisha juhudi za kuingiza TEHAMA katika lugha ya Kiswahili.

(h) Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki (BAKAMA)

(i) Kutetea na kuunga mkono kwa vitendo juhudi za kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki na hatimaye muungano wa Afrika ambao lugha yake kuu itakuwa ni Kiswahili.

Ili kufanikisha juhudi hizi, Kiango (2002) anapendekeza pawe na mpango wa mkakati utakaozingatia vipengele vyote vinavyusika. Tunakubaliana naye, na kuongeza kuwa mpango huo ingefaa uratibiwe na kuwa sehemu ya shughuli za msingi za sekretaria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tunahitimisha kwa kukumbusha kuwa Kiswahili kilienea, kinaenea, na kinadumu kwa kuwa kinahitajika. Kitakapokuwa hakihitajiki tena, kitakufa. Jukumu kubwa la wapenzi wa Kiswahili ni kuhakikisha kuwa kinaendelea kuhitajika ili kisife.

NYONGEZA

**Kisa cha kweli**

Nilisimuliwa kisa hiki na Mheshimiwa Kanyama Chiume, mwanasiasa na mpigania uhuru wa Malawi, tulipokutana Dar es Salaam tarehe 21 Septemba, 2001. Alisema: Mwezi Mei mwaka 1959 Rais Sekou Toure wa Guinea aliitisha mkutano wa viongozi wa vyama vyote vya kudai uhuru barani Afrika katika mji wa Conakry. Wajumbe walitoka katika nchi "zenye kuzungumza Kifaransa" na zile "zenye kuzungumza Kiingereza." Miongoni mwa wajumbe wa mkutano huo akikuwemo Chiume mwenyewe na Patrice Lumumba wa Kongo. Baada ya kuingia ukumbini, mkutano haukuweza kuanza kwa takriban saa 2; kisa – hapakuwa na mawasiliano! Wajumbe kutoka makoloni ya Kifaransa walifahamu lugha ya Kifaransa tu, lakini hawakujua Kiingereza. Na wajumbe kutoka makoloni ya Waingereza walifahamu lugha ya Kiingereza tu, hawakujua Kifaransa. Ilibidi Chiume aingilie kati na kupendekeza kuwa, madhali wajumbe

wa makoloni ya Waingereza na wale wa makoloni ya Wafaransa hawangaliweza kuwasiliana kwa lugha hizo, kwa nini wasitumie lugha ya Kiafrika kuondoa mgawanyiko huo wa bandia? Halafu akapendekeza Kiswahili kitumike kwa lengo hilo. Chiume alitoka Malawi na alifahamu Kiswahili na Kiingereza. Lumumba alitoka Kongo na alifahamu Kifaransa na Kiswahili. Iliamuliwa kuwa wajumbe kutoka makoloni ya Wafaransa waongee kwa lugha ya Kifaransa, Lumumba afasiri hotuba zao kwa Kiswahili, na Chiume alifasiri kwa Kiingereza. Halikadhalika, wajumbe kutoka makoloni ya Waingereza wazungumze kwa lugha ya Kiingereza, Chiume afasiri hotuba zao kwa Kiswahili, na Lumumba azifasiri kwa Kifaransa. Kwa kutumia njia hiyo, mkutano uliweza kuanza, na ukafanyika kwa mafanikio (Maelezo ya K. Chiume, Dar es Salaam, 21/9/2001).

Kisa hiki kinaeleza hali halisi ya nchi za Maziwa Makuu kuhusiana na lugha. Lugha tatu za wakoloni – Kifaransa, Kiingereza na Kireno zinazungumzwa katika ukanda huu. Wananchi walio wengi hawazifahamu lugha hizo, na wale wachache wanaozifahamu wanajua lugha mojawapo tu. Hivyo, Mganda anapotaka kufanya biashara na Mkongo hawezi kutumia Kiingereza au Kifaransa, itabidi atumie lugha kiungo, ambayo ni Kiswahili. Halikadhalika, Mtazania akitaka kuwasiliana na Mngazija au Mmsumbiji, hatotumia Kiingereza, Kifaransa, au Kireno, bali itabidi atumie Kiswahili, ambayo ndiyo lugha inayowaunganisha.

**Marejeo**


Armah, Ayi Kwei 1985 Our Language Problem. *West Africa* (Magazine). 29 April 1985, London: pp. 831-832.

Brock-Utne, B, Desai, Z na Qorro, M (Wah.) 2004 *Researching the Language of Instruction in Tanzania and South Africa.* African Minds, Cape Town.

Chiraghdin, Shihabuddin and Mnyampala, Mathias 1977 *Historia ya Kiswahili.* Oxford University Press, Nairobi.

Hurskainen, Arvi 1995 A Computer Archives of Kiswahili Language and Folklore: General Description, katika Mlacha na Hurskainen (1995: 1-15)

Khamisi, Abdu M 1974 Swahili as a National Language, katika Ruhumbika, G (Mh) *Towards Ujamaa,* EALB, Dar es Salaam: 288-230. Khamisi, Abdu M 1990 Swahili as a National Language, in Legère, K (ed): 95-114.

Kiango, J.G. 2002 Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii mpya ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies* Jz. 11/2: 185-197.

Kiango, J.G. 2005 Tanzania's Historical Contribution to the Recognition and Historical Development of Kiswahili. Katika *Africa & Asia 5* (Göteborg University): 157-168.

Kihore, Y & Chuwa, A.R (hakina tarehe); *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. TUKI (hakina tarehe).

King'ei , K Stunted Growth of Swahili Literature in Kenya: Causes and Remedy. *Kiswahili* 63: 89-95.

Legère, Karsten (ed) 1990 *The Role of Language in Literacy Programs with Special Reference to Kiswahili in Eastern Africa. A Contribution to the International Literacy Year.* DSE, BAKITA, Kenya Kiswahili Association, Goethe Institut-Nairobi. s of Kiswahili Development in Tanzania. Katika Shun'ya Hino (Mh) *African Urban Studies* II. 55-76. ILCAA, Tokyo university of Foreign Studies.

Massamba, D.P.B. 2002 *Historia ya Kiswahili 50-1500 BK.* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi. Massamba, D.P.B. 2004 Tanzania's Language Policy and Development: Language Experts vs Politicians. Katika National Institute of Japanese Language (NIJL) *Aspects of Foreign Words/Loan wors in the World's Languages.* NIJL, Tokyo: 333-344.

Mdee, J.S and Mwansoko, H.J.M (wah.) 2001: *Kongamano la Kimataifa: Kiswahili 2000: Preceedings.* TUKI, Dar es Salaam.

Mlacha, Shaaban A.K and Hurskainen, Arvi (eds) 1995 *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* TUKI, Dar es Salaam.

Mugambi, Peter J.M 1999 Language and Identity. *Chemchemi: International Journal of Arts and Social Sciences*, Faculty of Arts, Kenyatta University, Nairobi, pp. 114-117.

Mulokozi, Mugyabuso M 2000 Language, Literature and the Forging of a pan-African Identity. *Kiswahili* 63: 71-80.

Mulokozi,M.M 2003 Kiswahili as a National and International Language *Kiswahili* 66: 66-80. [Yanapatikana pia katika wavuti kupitia tovuti ifuatayo: www.helsinki.fi/hum/aakkl/documents/Kiswahili

Ohly, R 1982 Swahili - the Diagram of Crisis. University of Vienna/DUP, Dar es Salaam.

Tanzania 1984 Educational System in Tanzania Towards the Year 2000: Recommendations of the 1982 Presidential Commission on Education as Approved by the Pary and Government (Makweta Report). Government Printer, Dar es Salaam.

Tanzania (hakina tarehe: 1997?) *Sera ya Utamaduni*. Wizara ya Elimu na Utamaduni, Dar es Salaam.

Tanzania 1999 *Ripoti ya Mkutano wa Taifa wa Sera ya Utamaduni*. Wizara ya Elimu ya Utamaduni, Dar es Salaam.

Whiteley, W. 1969 *Swahili: The Rise of a National Language*. Methuen, London.